**HOTUBA YA MHE. JOEL ARTHUR NANAUKA (MB), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – MAENDELEO YA VIJANA, KATIKA HAFLA YA UTOAJI WA MIKOPO KUPITIA PROGRAMU YA SHILINGI BILIONI 200 CHINI YA MFUKO WA MAENDELEO YA VIJANA, WILAYA YA MBARALI, MKOA WA MBEYA TAREHE 12 JULAI, 2026**

- **Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa;**
- **Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Mbarali;**
- **Mheshimiwa Mbunge;**
- **Mheshimiwa Mwenyekiti wa Halmashauri;**
- **Wakuu wa Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi;**
- **Wawakilishi wa Taasisi za Fedha;**
- **Viongozi wa Vijana;**
- **Wanufaika wa Mikopo;**
- **Ndugu Wageni Waalikwa;**
- **Mabibi na Mabwana.**

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania...**

**Kazi na Utu...**

Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na neema, kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana siku ya leo katika hafla hii muhimu ya kuendelea kutekeleza Programu ya Shilingi Bilioni 200 chini ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Aidha, napenda kuwapongeza viongozi wote wa Mkoa wa Mbeya na Wilaya ya Mbarali pamoja na wadau mbalimbali waliofanikisha maandalizi ya hafla hii. Kipekee kabisa ninawashukuru sana **Benki ya CRDB** kwa kuwa sehemu ya wadau Wakuu

katika utekelezaji wa Programu hii. Ushirikiano wenu unaendelea kudhihirisha dhamira ya pamoja ya kuhakikisha vijana wanapata fursa zinazowawezesha kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya uchumi wa Taifa.

**Ndugu Wananchi;**

Kama mnavyofahamu, tarehe **09 Julai, 2026**, Serikali ilizindua rasmi utoaji wa Mikopo kupitia Programu ya Shilingi Bilioni 200 chini ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana katika Jiji la Arusha. Uzinduzi huo uliashiria mwanzo wa utekelezaji wa programu kubwa ya kitaifa inayolenga kuwawezesha vijana kupata mitaji yenye masharti nafuu ili waanzishe, waongeze na waendeleze shughuli za uzalishaji mali.

Leo hatufanyi uzinduzi mwingine; bali tunashuhudia hatua muhimu ya utekelezaji wa maamuzi yaliyofikiwa wakati wa uzinduzi huo. Serikali imeanza kutekeleza ahadi yake kwa vitendo kwa kuendelea kufikisha mikopo hii kwa vijana katika maeneo mbalimbali nchini. Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa inayonufaika katika hatua hii ya utekelezaji.

**Ndugu Wananchi;**

Mpango huu unatokana na maono thabiti ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** ambaye ameendelea kusisitiza kuwa maendeleo ya Taifa hayawezi kuwa endelevu bila kuwawezesha vijana kiuchumi. Chini ya uongozi wake, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya biashara, uwekezaji na upatikanaji wa huduma za kifedha kwa makundi mbalimbali ya wananchi, hususan vijana.

Vijana ndiyo nguvu kazi kubwa ya Taifa letu na msingi wa maendeleo ya uchumi wetu. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, takribani asilimia 34.5 ya Watanzania wana umri kati ya miaka 15 hadi 35. Hii ni rasilimali kubwa ambayo Serikali imeendelea kuiwekea mazingira bora ili iweze kuzalisha matokeo chanya kwa Taifa.

Ndiyo maana Serikali imeendelea kuweka maendeleo ya vijana kuwa miongoni mwa vipaumbele vya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 pamoja na Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007, Toleo la 2024, inayolenga kujenga kizazi cha vijana wanaojitegemea, wabunifu na washiriki wakuu wa maendeleo ya uchumi.

**Ndugu Wananchi;**

Changamoto ya upatikanaji wa mitaji imekuwa kikwazo kikubwa kwa vijana wengi wenye mawazo mazuri ya biashara na uzalishaji. Serikali imeendelea kutafuta suluhisho la kudumu kupitia Programu ya Shilingi Bilioni 200 ambayo sasa ipo katika hatua ya utekelezaji.

Kama ilivyoelezwa wakati wa uzinduzi uliofanyika Arusha, mwitikio wa vijana ulikuwa mkubwa ambapo maombi zaidi ya **30,000** yalipokelewa kutoka maeneo mbalimbali nchini yakihusisha sekta za kilimo, mifugo, uvuvi, viwanda vidogo, biashara, teknolojia na ubunifu. Takwimu hizi zinaonesha wazi kuwa vijana wa Tanzania wana ari kubwa ya kufanya kazi; wanachohitaji ni fursa na mitaji ya kuwawezesha kutekeleza ndoto zao.

**Ndugu Wananchi;**

Leo Serikali inaendelea kutekeleza programu hiyo kwa kutoa mikopo kwa vijana wa **Wilaya ya Mbarali, Mkoa wa Mbeya**, ambapo jumla ya **Shilingi 349,632,550** zinatolewa kwa vijana wanaojishughulisha na **sekta ya kilimo**.

Fedha hizi zitawawezesha kuongeza uzalishaji wa mazao, kutumia teknolojia za kisasa za kilimo, kuboresha tija mashambani, kuongeza thamani ya mazao yao, kupanua masoko na kuzalisha ajira zaidi kwa vijana wengine. Hii ndiyo dhamira ya Serikali ya kuhakikisha sekta ya kilimo inakuwa chanzo kikuu cha ajira, mapato na ukuaji wa uchumi wa Taifa.

Hatua hii pia inatekeleza kwa vitendo maelekezo na maono ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, ambaye ameendelea kusisitiza kuwa Tanzania haiwezi kufikia uchumi wa kati wenye ushindani endapo itaendelea kuuza mazao ghafi badala ya kuyaongezea thamani. **Mheshimiwa Rais** amekuwa akielekeza mara kwa mara kuwa vijana wanapaswa kuwa mstari wa mbele katika kuwekeza katika kilimo cha kisasa, usindikaji wa mazao, uhifadhi, vifungashio bora na matumizi ya teknolojia ili kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa nchini.

**Ndugu vijana wa Mbarali,**

Eneo lenu limebarikiwa kuwa miongoni mwa maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya kilimo nchini. Hivyo, mikopo mnayopokea leo isiishie kuongeza uzalishaji pekee, bali iwe chachu ya kujenga biashara zenye thamani zaidi. Mfikirie namna ya kuanzisha na kuimarisha shughuli za uchakataji wa mazao, kuongeza ubora wa bidhaa, kufungasha kwa viwango

vinavyokubalika sokoni na kutafuta masoko ya ndani na nje ya nchi. Hapo ndipo tutakapoongeza kipato cha wakulima, kuimarisha ushindani wa bidhaa za Tanzania na kutengeneza ajira nyingi zaidi kwa vijana.

Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi kupitia maboresho ya miundombinu, upatikanaji wa nishati, huduma za kifedha, masoko na mafunzo ya ujasiriamali ili kuhakikisha vijana wanaopata mikopo hii wanakuwa sehemu ya mabadiliko makubwa ya uchumi wa Taifa. Dhamira yetu ni kuona vijana hawabaki kuwa wazalishaji wa malighafi pekee, bali wanakuwa wajasiriamali na wawekezaji wanaoongeza thamani ya mazao, wanaojenga viwanda vidogo na vya kati, na wanaoshiriki kikamilifu katika kukuza uchumi wa viwanda jumuishi.

**Ndugu Wananchi;**

Napenda kutoa rai kwa viongozi wa Serikali, taasisi za fedha, sekta binafsi na washirika wa maendeleo kuendelea kushirikiana na Serikali katika kuhakikisha programu hii inasimamiwa kwa uwazi, uadilifu na uwajibikaji ili iweze kufikia malengo yaliyokusudiwa. Serikali itaendelea kufuatilia utekelezaji wa programu hii katika kila hatua na kuhakikisha fedha za umma zinatumika kwa manufaa yaliyokusudiwa.

**Ndugu Vijana;**

Nawasihi muendelee kutumia fursa zinazotokana na uchumi wa kidijitali, ubunifu na teknolojia kuongeza ushindani wa bidhaa zenu katika masoko ya ndani na nje ya nchi. Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya biashara, kuwajengea uwezo na kuendelea kupeleka mikopo hii katika maeneo mbalimbali nchini ili vijana wengi zaidi waweze kunufaika.

Lengo la Serikali ni kujenga kizazi cha vijana wanaojitegemea, wanaozalisha na wanaochangia kikamilifu katika maendeleo ya Taifa.

**Ndugu Wananchi;**

Kwa mara nyingine, napenda kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** kwa maono yake makubwa ya kuwawezesha vijana wa Tanzania kiuchumi.

Nina imani kuwa vijana wa Wilaya ya Mbarali watatumia vyema fursa hii na kuwa mfano wa mafanikio kwa vijana wengine nchini. Serikali itaendelea kutekeleza programu hii hatua kwa hatua katika mikoa na wilaya mbalimbali ili kuhakikisha vijana wengi zaidi wanapata fursa ya kujikwamua kiuchumi kupitia mikopo hii.

Baada ya kusema hayo, napenda kuwatakia kila la heri wanufaika wote wa mikopo ya leo na kusisitiza kuwa huu ni mwendelezo wa utekelezaji wa Programu ya Shilingi Bilioni 200 ambayo Serikali imeianzisha kwa ajili ya kuwawezesha vijana wa Tanzania.

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**

**Mungu ibariki Tanzania.**

**Mungu awabariki Watanzania wote.**